

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِتَسْتَقْبِلُهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَتَنَاهَى
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيَعْلَمُنَّ هُمْ وَيَهُمُ الظَّالِمُونَ أَرْضَنِي هُمْ وَلَيَعْلَمُنَّهُمْ مَنْ يَعْدُ حَوْفَهُمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بِهَذَا فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ



Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Ushirikiano wa Mamlaka za Uholanzi pamoja na Watu Ovyo wa Mayahudi Umesalia Kuvama ndani ya Kumbukumbu ya Umma... (Imetafsiriwa)

Vyombo vya habari vya kimataifa vimeripoti vitendo vya kundi la wachochezi wa Kiyahudi wakati na baada ya mechi ya kandanda, kujihusisha na uchokozi dhidi ya Waislamu kuhusiana na kadhaa kuu ya Umma wa Kiislamu, kadhaa ya Palestina. Vitendo hivi viliibua hisia za kimaumbile kutoka kwa Waislamu wa mataifa mbalimbali na kutoka kwa raia waheshimiwa wa Uholanzi wenywewe. Hata hivyo, kinachodhahirika ni kimya cha mamlaka za Uholanzi kuhusiana na chokochoko za wachochezi hao, ikifatiwa na vyombo vyao vya usalama kukabiliana na waandamanaji wanaopinga chokochoko hizi na kuwakamata wengi wao!

Katika muktadha wa majibu, misimamo fulani ya fedheha inafaa kutajwa. Tukianza na kauli ya Waziri Mkuu wa Uholanzi Mark Rutte, ambaye alilaani kile alichokitaja kuwa "mashambulizi dhidi ya Mayahudi." Vile vile, Balozi wa Marekani katika umbile la Kiyahudi alishutumu kile alichokitaja kama "mashambulizi ya kutisha" dhidi ya Mayahudi, akipuuza kiurahisi kwamba ni wao walioanzisha uchochezi na vitendo vya ghasia. Jambo la kuchukiza vile vile ni matamshi ya Mjumbe Maalum wa Marekani wa Ufuatilaji na Kupambana na Chuki dhidi ya Mayahudi, ambaye alionyesha kushtushwa na kile alichoeleza kuwa mashambulizi yaliyotokea Amsterdam. Rais wa Tume ya Muungano wa Ulaya pia alionyesha kukasirishwa na kile alichokiita "mashambulizi ya kuchukiza" yaliyolenga Mayahudi jijini Amsterdam. Charles Michel, Rais wa Baraza la Ulaya, alisitiza ahadi yake ya kupambana na chuki dhidi ya Mayahudi, kama alivydai. Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani Annalena Baerbock alitaja matukio hayo kutoka Amsterdam kuwa "ya kutisha na ya aibu sana kwa Ulaya." Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, kwa upande wake, alitumia fursa hiyo kukumbuka nyakati za giza zaidi katika historia, akimaanisha kile alichokiita ghasia dhidi ya mashabiki wa soka wa Kiyahudi.

Haya yote—kwa tukio lolote au pasi kwa tukio—yanathibitisha uadui wao dhidi ya Uislamu na Waislamu, bila ya haki wanaunga mkono wahalifu wavamizi ambaa wameteka ardhi iliyobarikiwa ya Palestina, wakipuuza kwa urahisi—au wakipuuza kwa makusudi—uhalifu wa Mayahudi nchini Palestina na kwengineko, uhalifu unaotendwa dhidi ya watoto, wanawake na wazee. Umbile lao katili iliundwa juu ya mafuvu ya Waislamu, kuanzia Nakba ya 1948 na kuendelea na ukatili wao wa hivi karibuni huko Gaza, Lebanon, Syria, Iraq, Yemen na Iran.

Ingawa tunapongeza misimamo ya watu wengi waheshimika na walio huru barani Ulaya ambaa wamesimama dhidi ya uhalifu wa hivi karibuni wa umbile la Kiyahudi huko Gaza na chokochoko za wachochezi wa Kiyahudi, ujumbe wetu unaelekezwa kwa serikali na mamlaka barani Ulaya na kwengineko - haswa zile ambazo ziliunga mkono misukosuko ya uchafu wa Kiyahudi, ziekigemea upande wa umbile la Kiyahudi katika unyakuzi wake wa ardhi za Waislamu, na zilichangia kuundwa kwa umbile hilo. Kwa yale mataifa yote ambayo yamesaidia mauaji na jinai zake, tunasema: ukatili wote huu umebakia kuvama ndani ya kumbukumbu ya Umma wa Kiislamu na hautasahafulika kamwe. Mataifa haya hayatakuwa na hadhi wala mapatano na Ummah wakati Khilafah ijayo, itakaposimamishwa hivi karibuni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, kuliondoa umbile la Kiyahudi kutoka uwepo.

[وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَبٍ يَنْقَبُونَ]

"Na wanao dhulumu watakuja jua mgeuko gani watakao geuka." [Ash-Shu'ara:227].

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir



Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

www.hizb-ut-tahrir.org

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

www.hizb-ut-tahrir.info